

**M**begu kutoka sekta ya biashara kwa kawaida ni chotara, Mbegu bora Zilizopevushwa Kiasili na aina nyingine ya vipandikizi kama vile miche. Hizi huzalishwa na makampuni binafsi na taasisi za utafiti, na pia hujulikana kama **mbegu bora**.

**Mbegu chotara** ni mbegu ya kizazi cha kwanza iliyozalishwa kupitia mchanganyiko wa koo mbili ambazo hazihusiani kiasili. Ili kuzalisha mbegu chotara, mchakato wa uchavushaji lazima udhibitiwe kwa makusudi au kuelekezwa. Mbegu chotara kwa sehemu kubwa hutayarishwa na makampuni ya mbegu. Ni mbegu ghali na lazima zinunuliwe kila msimu, hivyo kuongeza utegemezi wa wakulima kwenye makampuni ya mbegu. Wakulima wanapopanda mbegu chotara walizohifadhi kutoka shamba, mavuno yanakuwa chini.


**Mbegu bora Zilizopevushwa Kiasili** ni mbegu ambazo zimeendelezwa kwa muda mrefu kupitia uzalishaji wa wazi na huwa na wigo mpana wa sifa zinazofanana kama vile uzito, ukubwa na unene sawa. Kwa kawaida si lazima wakulima wanunue mbegu hizi kila msimu, zinaweza kurudiwa kupandwa bila ya kupoteza mavuno.

**Vipandikizi** vinatokana na sehemu ndogo ya mmea asilia – kama vile majani na shina lililokatwa, vichipukizi na mitaambazi – ambavyo mimea mipya huweza kuzalishwa.

# MBEGU KUTOKA SEKTA YA BIASHARA



benki ya vinasaba




udhibiti wa ubora



uzalishaji wa mbegu



mbegu ya mzalishaji



Mbegu bora na vipandikizi huweza kuzalishwa kwa wingi kwa mzalishaji wa mmea kutoa leseni kwa makampuni ya mbegu kufanya hivyo. Mbegu iliyozalishwa kwa wingi kwa njia hii huitwa **mbegu iliyothibitishwa**. Wakati mwingine wakulima pia hupewa mkataba wa kuzalisha kwa wingi mbegu iliyothibitishwa. Uzalishaji mbegu kwa wingi hufanyika kwa kuzingatia viwango vikali vilivyowekwa katika Sheria ya Mbegu.

Wazalishaji pia wanaweza kutoa leseni kwa makampuni ya mbegu kuzalisha mbegu iliyothibitishwa, ambao wanaweza pia kuiuza kwa wakulima. Mbegu hii ni ghali sana na huzalishwa mavuno mazuri iwapo tu wakulima wataitumia pamoja na mbolea na viuadudu vya kemikali.

